



## LOWELL PUBLIC SCHOOLS

Henry J. Mroz Central Administration Offices  
155 Merrimack Street  
Lowell, MA 01852

Juni 3, 2020

Shule ya Lowell Public Schools ina furaha kutangaza wagombea watatu wa mwisho wanaozingatiwa kuchukua Jukumu la Mkuu wa Shule katika Shule ya Upili ya Lowell High School (waliorodheshwa hapa chini katika mpangilio wa alfabeti):

- **Ian Charles** hivi karibuni alihudumu kama mwalimu mkuu katika shule ya Codman Academy, shule ya jamii katika Dorchester. Alianza kazi kama mwalimu katika shule ya Lowell Public Schools na akaendelea ualimu katika jimbo la Florida, kabla ya kurudi Massachusetts. Aliendelea kuhudumu kama msaidizi wa mwalimu mkuu na mwalimu mkuu wa shule katika Massachusetts. Kwa sasa ni mwanafunzi wa phd katika Chuo Kikuu cha Northeastern University katika Idara ya Masomo ya Kitaaluma au College of Professional Studies katika uongozi wa usimamizi.
- **Michael Fiato** huhudumu kama Targeted Assistance Manager (Msimamizi wa Usaidizi Uliyolengwa) katika Statewide System of Support (Mfumo wa Usaidizi wa Jimbo zima) ya Idara ya Elimu ya Kimsingi na ya Upili au Department of Elementary and Secondary Education. Kabla ya kujiunga na DESE, alihudumu kama mwalimu mkuu wa shule ya upili ya Lawrence High School, na kabla ya hapo alikuwa mwalimu mkuu katika moja ya shule sita za Lawrence High.
- **Dr. Sara P. Walsh** kwa sasa huhudumu kama mwalimu mkuu wa shule ya upili ya Algonquin Regional High School. Ana leseni ya kufundisha katika biyolojia na hesabu, iliyo na zingatiao zaidi ya fisiolojia. Pia amehudumu katika jukumu la Mwalimu mkuu Mshiriki, Msaidizi wa Mwalimu Mkuu, na Mwalimu Mkuu katika shule za Springfield Public Schools.

Wasifu kamili wa kila mgombea imechapishwa hapa:

<https://www.lowell.k12.ma.us/LowellHighHeadofSchoolFinalistsBio>

Wilaya itaandaa mikutano mitatu ya kijamii kwa mtandao wiki ijayo, ili kuwapatia fursa umma kukutana na wagombea wote na kuuliza maswali kuhusu historia yao na maono yao kwa shule ya Lowell High.

- Jumanne, Juni 9 kutoka 5 jioni hadi 6 jioni
- Jumatano, Juni 10 kutoka 5 jioni hadi 6 jioni
- Alhamisi, Juni 11 kutoka 5 jioni hadi 6 jioni

Viunga vya mtandao vya Zoom za mikutano hizi zitachapishwa katika tovuti na mtandao wa jamii wa wilaya mnamo Jumatatu, Juni 8, 2020. Iwapo ungependa kuuliza swali, tafadhali tuma swali lako kabla ya mkutano wa jamii ukituma barua pepe kwa anwani [community@lowell.k12.ma.us](mailto:community@lowell.k12.ma.us). Tarehe la mwisho la kutuma swali ni Jumanne, Juni 9, 2020 adhuhuri.

Kwa ujumla, watu 22 walituma ombi kwa kazi hii. Kamati ya Kutafuta ya Lowell High School – inayowakilisha wanakamati tofauti wakiwamo wanafunzi, wazazi, walimu, wasimamizi, na washiriki wa kijamii – walitambua na kuwafanya mahojiano wagombea 12, kabla ya kuchagua wagombea watatu wa mwisho. Kamati ya Kutafuta ilipatiwa kazi ya kutathmini maelezo ya kazi, kushughulika mwelekeo wa kutopendelea, kutathmini maoni kutoka utafiti wa kijamii, kuandaa maswali ya mahojiano, kutathmini vyombo vya kufanya maombi ya kazi na kupendekeza wagombea watatu wa mwisho.

Wanachama katika Kamati ya Kutafuta:

- Wanafunzi: Jaeda Turner & Princess-Henna Wilson
- Wazazi: Heather Forythe, Luis Raudales, Brian Snow
- UTL (United Teachers of Lowell (Muungano wa Walimu wa Lowell)): Nancy Connelly, MaryAnn Dyson, Kristen Schultz
- LSAA (Lowell School Administrators Association (Muungano wa Wasimamizi wa Shule wa Lowell)): Deidre Haley & Rose Mendoca
- SEIU (Service Employees International Union (Umoja wa Kimataifa wa Wafanyikazi wa Huduma)): Joan Marias
- Higher ED Partners (Washiriki wa Elimu ya Juu): Dr. Ellen Grondine, MCC & Dr. Phitsamy Uy, UML
- Shirika la Jamii: LZ Nunn, Mradi wa LEARN
- Mwanachama wa Kamati ya Shule: Hilary Clark, Personnel Chair
- Wawezeshaji wa LPS: Linus J. Guillory Jr., PhD & Daroth Yann, HR

Baada ya mikutano ya kijamii kufanyika, shughuli itakamilishwa na mahojiano ya mwisho na Dr. Joel Boyd, Msimamizi Mkuu wa Shule za Lowell Public Schools.